OFISI YA RAIS –TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA
SHULE YA SEKONDARI BUMILAYINGA

BUMILAYINGA SEKONDARI,
S.L.P.429,
MAFINGA-IRINGA.
06.12.2020

-Email:albert.mkollo @mafinga tc. go. tz

SIMU:0755-200580/0621-109-845

KUMB.NA.BSS/S.3470/SJI/VOL/13

JINA LA MWANAFUNZI ..............................................................................

## 1.0 UTANGULIZI.

Shule ya sekondari bumilayinga inayofuraha kukukaribisha kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka wa masomo 2021.Ninakupongeza sana kwa kufanya mitihani yako ya darasa la saba vizuri mwaka 2020 na hivyo kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2021.

Shule hii ipo umbali wa KM 25 Kusini Magharibi mwa Halmashauri ya Mji Mafinga.Usafiri wa basi kutoka Mafinga Mjini unapatikana wakati wowote eneo la Mafinga jirani na NMB nauli ni Tsh.2000 tu. Muhula wa kwanza , masomo yataanza 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni 17.01.2021 ndani ya siku saba.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 1 SARE ZA SHULE.

a) Sare ya shule hii ni suruali nyeusi na mashati meupe mikono mirefu kwa wavulana na sketi nyeusi kwa wasichana
b) Rangi ya hijab ifanane na sare ya za shule.
c) Sare za michezo ni bukta,viatu au raba na fulana kwa wavulana na traksuti nyeusi kwa wasichana
d) Daftari kumi na mbili (counter books) na mkebe pamoja na kalamu.
e) Viatu vyeusi vya kamba kwa wote (wavulana na wasichana) short stockings na soksi nyeupe.
f) Sweta rangi ya bluu,rangi nyingine ya sweta au koti hautaruhusiwa kuvaa shuleni

### 2. NIDHAMU

- Makosa yanayoweza kumsababishia mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:

i)wizi
ii)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama bagi, mirungi, kuberi,cocaine nk.
iii)Ubakaji, uasherati na ushoga
iv)kupiga au kupigana
v)kuoa au kuolewa, kupata mimba au kusababisha mimba, kutoa mimba
vi)kuwa na simu ya mkononi eneo la shule
vii.)kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama shuleni

viii)Kukataaa adhabu kwa makusudi

3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NAKUWASILISHWA SHULENI SIKU YA KURIPOTI

I.Fomu ya daktari (medical examination form)ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali

ii)Fomu ya mzazi ya kukiri na kukubari sheria

iii)Fomu ya maelezo binafsi ya historia ya mwanafunzi

KWA WATAKAO ISHI HOSTEL VIFAA VYA CHAKULA NA VYOMBO VINGINE IFUATAVYO:-

| VIFAA | IDADI |
|---|---|
| Sahani | 1 |
| Kikombe | 1 |
| Bakuli | 1 |
| Ndoo ndogo ya plastic kwa hosteli | 1 (10lts) |
| Kijiko | 1 |
| Godolo ft 2.5 | 1 |
| Blanketi | 1 |
| Shuka rangi ya blue bahari | 1 |
| Mto na foronya | 2 |
| Chandarua | 1 |
| Kanga au kitenge | 1 pair |
| Taulo | 2 |
| Tracksuit | 1 |
| Gauni ya rangi ya blue isiyo na marinda tafadhali shona | 1 |

4.1 UCHANGIAJI CHAKULA KWA WANAFUNZI WA HOSTEL

i.Uchangiaji wa chakula ni jukumu la wazazi hii ni kwa maelezo yaliyotolewa na serikali kwa wasichana wa hostel na day (kutwa chakula cha mchana ni kwa wote.

ii)Chakula kitalipwa kwa awamu, hivyo kitalipwa mihula miwili tu. Tafadhali zingatia hilo.

ANGALIZO:

a)HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA MZAZI /MLEZI AMBAYE HATA MLETA MWANAE SHULENI.

b)MWANAFUNZI AKIVUNJA KITI, MEZA, KUHARIBU MIUNDO MBINU YA SHULE, MZAZI ATALAZIMIKA KURUDISHIA KAMA ILIVYOKUWA AWALI. HAKUNA KUCHORA KUTAWALA CHOCHOTE KATIKA ENEO LA SHULE.

KARIBU BUMILAYINGA SEKONDARI

..............................

ALBERT JOHN MKOLO

MKUU WA SHULE